



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI



NAMBA ZA SIMU

MKUU WA SHULE: 0783009294

M/MKUU WA SHULE: 0755067244

MHASIBU: 0766166828.

MATRON: 0766299144

SHULE YA SEKONDARI IKUNGI,
S. L. P 953,
SINGIDA.

TAREHE:.....

KUMB. Na. IKSS/JOINING INSTR/F. V – 2024

MWANAFUNZI _____,

S. L. P _____,

_____.

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKUNGI KIDATO
CHA TANO, HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA
SINGIDA MWAKA 2024.**

1.0. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiungana kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 tahasusi ya..... Shule ya sekondari Ikungi ipo umbali wa Kilometa 0.1 au mita 100 magharibi mwa mji wa Ikungi. Usafiri wa basi kutoka mjini SINGIDA unapatikana katika kituo cha mabasi kilichopo karibu na stendi kuu na nauli ni Tshs 3000/= kwa wale watakaotoka kanda ya ziwa, Arusha, na Moshi. Lakini wale wanatokea barabara ya Dar Es Salaam watashukia stendi ya Ikungi mjini ambayo ipo karibu na shule.

Muhula wa masomo utanza tarehe ___/___/2024 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ___/___/2024 mwisho wa kuripoti ni tarehe ___/___/2024

2.0. MAMBO YA KUZINGATIA.

2.1. SARE YA SHULE.

- (i) Sare ya shule hii ni sketi ya **JANI LA MGOMBA** yenye marinda 8 hadi 16 na unatakiwa kushona sketi ndefu yenye urefu 34 kwa wale wafupi na wale warefu, urefu iwe 36 na isiwe ya rinda boksi. Ili kuepuka kukosea rangi na namna ya ushonaji itakayopelekea hasara kwa mzazi kushona sare mara mbili, sare hii inapatikana shuleni kwa atakayehitaji yaani sketi kwa Tsh 24,000/= kwa sketi moja na unatakiwa kushona sketi mbili. Kwa mawasiliano 0676168747.
- (ii) Sweta ni **JANI LA MGOMBA** lisilo na mistari yeyote, pia kwa atakayehitaji inapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=.
- (iii) Shati 2 nyeupe za tomato zenye mikono mirefu hivyo mzazi unatakiwa kununua.
- (iv) Kwa wale waislamu rangi ya hijabu (kijuba) iwe nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

- (v) Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta ya bluu, T shirt ya bluu na raba nyeupe.
- (vi) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi.
- (vii) Soksi jozi mbili nyeupe ndefu.
- (viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni sketi ya rangi NYEUSI yenye marinda 8 hadi 16 na tracksuit ya kijivu yenye mistari mieupe pembeni zisizo na kofia. Kwa sketi unashauriwa kushona sketi ndefu yenye urefu 34 kwa wale wafupi na wale warefu, urefu iwe 36 na isiwe ya rinda boksi, pia kwa atakayehiji inapatikana shuleni kwa Tsh 24,000/= kwa sketi moja.
- (ix) Mwanafunzi anatakiwa kuja na T-shirt mbili za njano zenye kola zenye mistari mieusi kwenye kola, mkononi, na mfukoni wakati wa kuripoti, kwa atakayehitaji inapatikana karibu na shule kwa Tsh 15,000/= kwa T-shirt moja, kwa atayekuja na T-shirt aje na Tsh 5,000/= kwa kila T-shirt kwa ajili ya nembo.

2.2. MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI NI:-

Na	Aina ya Mchango	Kiasi
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo kwa ajili ya shati	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	Jumla	80,000/=

MUHIMU:

- Kila mwanafunzi anatakiwa aje na bima ya afya (NHIF) au CHF wakati wa kuripoti ili awe anaitumia katika matibabu. Pia kwa mbao hawana BIMA aje na Tshs. 5,000/= kwa ajili ya BIMA ya CHF iliyoboresha.

Fedha hizo za michango zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na **50801100027** jina la akaunti ni **IKUNGI SECONDARY SCHOOL** katika benki ya **NMB** na mwanafunzi aje na Pay in slip ILIYOANDIKWA JINA LAKE NA MCHANGANUO WAKE. (MICHANGO ILIPWE YOTE)

2.3. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

- Ream 2 A4 ya karatasi kwa mwaka.
- Godoro lenye upana wa $2^{1/2}$ futi 6 na unene nchi $2^{1/2}$
- Mashuka pair mbili rangi ya bluu bahari, Blanket 1, mto wenye foronya 1 rangi ya bluu bahari, chandarua rangi ya bluu 1 na taulo 1
- Vyombo vya chakula ni sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko (ndoo 1 atakabidhi, ndoo nyingine kwa ajili ya matumizi yake)
- Galoni ya lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa (zinapatikana shuleni kwa Tsh 2500/=)
- **Vitabu vya masomo Tahasusi ni kama ifuatavyo:**

❖ **ECONOMICS:**

Ambilikile paper 1 & 2 au ZIST KAMILI paper 1 & 2

❖ **BASIC APPLIED MATHEMATICS. (kwa wanafunzi wa HGE)**

(i) Additional and Applied Mathematics by J. F. TALBERT

- (ii) Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
- (iii) Basic applied mathematics review questions and solutions
- (iv) BASIC APPLIED MATHEMATICS for Secondary Schools: Form five and Six (TIE)

❖ **GEOGRAPHY:**

- (i) Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman.
- (ii) Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D.
- (iii) Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa, Longman.
- (iv) Kamili, A Comprehensive Approach Practical Geography For Advanced Level, Dar es salaam, Afroplus Industries.
- (v) Kamili, Physical Geography for Africa, Dar es salaam Afroplus Industries.
- (vi) Msabila D.T. Physical Geography, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
- (vii) Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

❖ **KISWAHILI:**

- (i) Sarufi ya Kiswahili Sekondari na vyuo (MDEE) NA KISW. 1 Nadharia ya lugha kidato cha 5 & 6 (SALUHAYA, C)
- (ii) J.A. MASEBO na M. Nyangwine, Nadharia ya Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.
- (iii) H.J.M. Mwasiko, R.D.K. Mekacha, D.L. Masoko, P.C.K. Mtengwa; Kitanglizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu.
- (iv) Tahakiki kidato cha tano na sita.
- (v) Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II.
- (vi) Kiswahili – I: Mwandishi Masuko Christopher Saluhaya.
- (vii) Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu. Wandishi: - H.J.M. Mwansoko, R.D.K. Makacha, S.L.W. Masoko, P.C.K. Mtengwa.
- (viii) Kiswahili Sekondari – Kidato cha Tano (TIE)
- (ix) Kiswahili Sekondari – Kidato cha Sita (TIE)

❖ **HISTORY:**

HISTORY ONE

- (i) Webster J.B. The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years of West Africa Siche 1800, Longman Press.
- (ii) Walter Rodney, How Europe Underdeveloped Africa.
- (iii) Hallert, R. (1983). Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.
- (iv) July, R.W. (1992). A History of the African People, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
- (v) Illife, J. (1995). Africans, the History of the Continent. Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
- (vi) Manning, P. (1990). Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade, Cambridge University Press.

- (vii) Njiro, E. (1989). A History of Africa in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
- (viii) Rodney, W. (1976). How Europe underdeveloped Africa, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
- (ix) Shillington, K. (2004). History of Africa. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
- (x) Davidson, E. et al (1997); The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore.
- (xi) Freud, B. (1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
- (xii) Kimambo, I and Temu, A (1969); A History of Tanzania, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
- (xiii) Robin, H. (1993); African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd, Nairobi, Kenya.
- (xiv) Roland, O. and Anthony, A. (2007). Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.
- (xv) History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
- (xvi) History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
- (xvii) History for secondary schools: Form Five (TIE)

HISTORY TWO

- (xviii) Nelson throne Essential modern world history
- (xix) History of 21st century (World history) (Oxford)
- (xx) H.L. Peacock. A History of Modern Europe 1789-1981 seventh Edition (2010)
- (xxi) The History of Modern World (2007) 6th Edition by Oxford University Press
- (xxii) History two for advanced level by Idris Ramadhani Msuya.

❖ ENGLISH LANGUAGE:

VITABU VYA LANGUAGE (1) ONE: -

- (i) Advanced level English structure and stylistic 4th Ed by Nicholus Asheli,
- (ii) Nichlolus arshery, Comprehensive English Grammar New edition.
- (iii) Michael Kadegehe, Sematics phonology and styhstics. (blue).
- (iv) Ashel, N. (2009) Advanced Level English A Practical Approach. DSM.
- (v) Kadegehe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form Six) – DSM
- (vi) Kadegehe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced Level (form five) – DSM.
- (vii) English Language for Secondary Schools, Language & Usage – Form Five & /six (TIE) papers.
- (viii) Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

LANGUAGE (II)

- (ix) Ashel, N. (2011), Advanced Level Literature. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.
- (x) Advanced Level Literature, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.
- (xi) Achebe, A. (1966) A man of the People.

- (xii) Ayi Kwei Armah (1968), The Beautiful Ones Are Not Yet Born.
- (xiii) Ibsen, H. (1882), An Enemy of the People, EA-DSM
- (xiv) Imbuga, FC (1976) Betrayal in the City.
- (xv) Mirii Ngugi & Thing'ol (1982), I Will Marry When I Want, EAEP, DSM.
- (xvi) Institute of Education, Selected Poems.
- (xvii) Mloka, C. (2007) The Wonderful Surgeon.
- (xviii) English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics – Form Five & Six (TIE). Paper 2.

❖ **GENERAL STUDIES: -**

- (xix) General studies Approach.
- (xx) Richard, R.F. Mbalase. General Studies for Advanced Level Certificate;
- (xxi) Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3 rd Ed.
- (xxii) Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies; Advance Secondary School Education;

❖ **SCIENTIFIC CALCULATOR**

2.4. VIFAA VYA USAFI VILETWE KWA KUZINGATIA MAELEKEZO YA KILA TAHASUSI (COMBINATION) KAMA IFUATAVYO

- **HGL** wataleta Jembe 1, soft broom 1, chelewa 1, ndoo ndogo 2, Brush za chooni 1, sabuni ya maji lita tano, squeezer 1 na panga 1
- **HGK** wataleta Jembe 1, soft broom 1, chelewa 1, ndoo ndogo 2, Brush za chooni 1, sabuni ya maji lita tano, squeezer 1 na panga 1
- **HGE** wataleta Jembe 1, soft broom 1, chelewa 1, ndoo ndogo 2, Brush za chooni 1, sabuni ya maji lita tano, squeezer 1 na panga 1
- **HGLi** wataleta Jembe 1, hard broom 1, chelewa 1, ndoo ndogo 2, Brush za chooni 1, sabuni ya maji lita tano, squeezer 1 na panga 1
- **HGFa** wataleta Jembe 1, hard broom 1, chelewa 1, ndoo ndogo 2, Brush za chooni 1, sabuni ya maji lita tano squeezer 1 na panga 1

3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

3.1. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- (i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- (ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- (iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
- (iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- (v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- (vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- (vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- (viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

- (ix) Kutunza mali za shule;
- (x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- (xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

3.2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

- (i) Wizi;
- (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- (vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
- (vii) Kufuga ndevu;
- (viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
- (ix) Uvutaji wa sigara;
- (x) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuo au kuolewa;
- (xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- (xii) Kusababisha mimba;
- (xiii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- (xiv) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- (xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- (xvi) Kudharau Bendera ya Taifa;
- (xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- (xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4.0. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

- (i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- (ii) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

- (iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- (iv) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

MUHIMU:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule:** 0783009294
- **Makamu Mkuu wa Shule:** 0755067244
- **Mwandamizi Taaluma:** 0753260016
- **Matroni (mwalimu mlezi):** 0766299144

Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKUNGI


NEEMA T. STEPHANO

MKUU WA SHULE

**HEADMISTRESS
IKUNGI SEC. SCHOOL
P.O.Box 988 SINGIDA**



**PRESIDENT'S OFFICE,
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL
GOVERNMENT**



**IKUNGI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 953,
SINGIDA.**

- A. MEDICAL EXAMINATION FORM** Year
- To be completed by a medical officer in respect of all form I – VI entrants and New school employee.

**TO THE MEDICAL DOCTOR..... HOSPITAL/HEALTH CENTRE BOX
.....**

Please Examine Age Whether is fit to pursue studies/work

Test for

Blood (Red and white)

Stool examination.....

Urinal.....

Syphilis.....

T.B.....

Eye

Ear.....

Chest

Abdomen.....

- B. ADDITIONAL INFORMATION:** Physical defects important, infection or family diseases act.....

- C. I certify that the above mentioned student is fit to pursue studies**

Medical Doctor's Signature.....

Name.....

Designation.....

Station.....



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



FOMU YA KUKUBALI

(Fomu hii pamoja na fomu ya afya irudishwe shuleni siku ajapo mwanafunzi)

MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi _____ msichana/mvulana nimekubali kujiunga kidato
Cha _____ shule ya sekondari Ikungi tarehe _____ nitafika
shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria na nitaishi maisha mazuri na nitakuwa
mwanafunzi Mwenye bidii kwenye masomo na kazi za nje. Sitashiriki katika
mgomo, fujo na Makosa ya jinai
2. Kama sitatimizâ sheria na kanuni muhimu za shule hii naomba küchukuliwa hatua
za kinidhamu hii ni pamoja na kufukuzwa shule kwa makosa yasiyovumilika.

MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi _____ Nimekubali mtoto wangu (Jina)
_____ Asume katika shule ya sekondari Ikungi kuanzia
_____ naahidi kumpatia vitu vyote vinavyotakiwa kufika navyo
shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule
2. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria zote za shule
nakuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi. Nakiri nitalipa
michango iliyoainishwa na sitaleta usumbufu kwa mwanangu na kwa uongozi wa
shule.
3. Anwani yangu ya kudumu ni _____
Simu _____
Sahihi _____ Tarehe _____

Wageni ninaowaidhinisha kumwona mtoto wangu awapo shuleni

- i) uhusiano wake
- ii) uhusiano wake
- iii) uhusiano wake
- iv) uhusiano wake



